JIMBO KATOLIKI LA MOROGORO
ALFAGEMS SECONDARY SCHOOL (S.3874)
S.L.P. 6083 – MOROGORO
Tel. 0732-931605 (ofisi) / 931697 (bweni la kike)
www.alfagems.com

NAFASI ZA MASOMO

- Shule yetu inazingatia taaluma na maadili kwa kufuata sera ya elimu ya Kanisa Katoliki.
- Tunawashukuru nyinyi, wananchi wote, kwa kuonyesha mmeipenda sana.
- Pamoja na kuahidi juhudi endelevu za kuboresha huduma, tunafurahi kuwatangazia nafasi 12 zifuatazo.
- Kila nafasi ina fomu maalumu kadiri ya namba zifuatazo.
- Kabla hamjanunua fomu inayohusika, chagueni vizuri masomo mnayoyahitaji.
- Baadaye hamtaruhusiwa kubadili fomu wala masomo, kwa sababu ni lazima twende kimpango.

MASOMO YA KUANZIA ASUBUHI

1. **KUJIANDAA MIEZI MITATU KWA KIDATO CHA KWANZA** (English na Mathematics). Kozi hii haimpi mwanafunzi haki ya kuchaguliwa asome kidato cha kwanza. Masomo yataanza tarehe 3-10-2011. Ada ni Tsh. 40,000. Kwa kukaa bweni, wasichana wataongeza Tsh. 80,000.
2. **KUINGIA KIDATO CHA KWANZA** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics). Wanaotaka kujiunga wawe wamezaliwa si kabla ya mwaka 1994 na kufaulu mtihani wa darasa la saba mwaka 2010 au 2011. Tofauti na hayo, mtu afikirie namba 6 au 7 hapa chini. Usaili utafanyika tarehe 19-11-2011 na 17-12-2011 saa 3:00 asubuhi. Masomo yataanza tarehe 3-1-2012. Ada ni Tsh. 200,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni, wasichana wataongeza Tsh. 300,000, wavulana Tsh. 360,000.
3. **KUHAMIA KIDATO CHA PILI, CHA TATU AU CHA NNE** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology, Chemistry, Physics na Mathematics; au Civics, History, Geography, English, Literature, Kiswahili, Biology, na Mathematics). Wanaotaka kujiunga wawe wamefanya vizuri (walau 50%) katika masomo ya kidato cha chini katika shule yoyote iliyosajiliwa. Tofauti na hayo, mtu afikirie namba 6-8 hapa chini. Usaili utafanyika tarehe 10-12-2011 saa 3:00 asubuhi. Masomo yataanza tarehe 3-1-2012. Ada ni Tsh. 200,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 300,000, wavulana Tsh. 360,000.
4. **KUINGIA KIDATO CHA TANO** (History, Kiswahili na Language; au History, Geography na Kiswahili; au History, Geography and Langage; au History, Geography na Economics; au Physics, Chemistry na Biology; au Chemistry, Biology na Geography). Wanaotaka kujiunga wawe wamepasi (A, B, C au D) walau masomo matano (yakiwemo English na yale waliyoyachagua) na kupata credits (A, B au C) walau tatu katika masomo yoyote walipofanya au kurisiti mtihani wa kidato cha nne. Wawe wamezaliwa si kabla ya mwaka 1990 na kupata credit ya tatu mwaka 2011 au 2012. Tofauti na hayo, mtu afikirie namba 11-12 hapa chini. Masomo yataanza tarehe 10-4-2012. Ada ni Tsh. 240,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 300,000.
5. **KUHAMIA KIDATO CHA SITA** (History, Kiswahili na Language; au History, Geography na Kiswahili; au Physics, Chemistry na Biology). Wanaotaka kujiunga wawe wamefanya vizuri (walau 50%) katika masomo ya kidato cha tano katika shule yoyote iliyosajiliwa. Usaili utafanyika tarehe 30-3-2012. Masomo yataanza tarehe 10-4-2012 saa 1:30 asubuhi. Ada ni Tsh. 240,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 300,000.

MASOMO YA KUANZIA ALASIRI (JUMAMOSI KUANZIA ASUBUHI)

6. **KUJIANDAA MWAKA MZIMA KWA MTIHANI WA MAARIFA = Q.T.** (Civics, History, Geography, English na Kiswahili). Masomo yataanza tarehe 18-10-2011. Ada ni Tsh. 160,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 340,000.
7. **KUJIANDAA MIAKA MIWILI KWA MTIHANI WA MAARIFA = Q.T.** (Civics, History, Geography, English, Kiswahili, Biology na Mathematics). Masomo yataanza tarehe 10-1-2012. Ada ni Tsh. 140,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 300,000.
8. **KUJIANDAA MIAKA MIWILI TENA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE** (Civics, History, Geography, English, Literature, Kiswahili, Biology na Mathematics). Wanaotaka kujiunga wawe na elimu inayolingana walau na ile ya kidato cha pili. Masomo yataanza tarehe 21-2-2012. Ada ni Tsh. 120,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 260,000.
9. **KUJIANDAA MWAKA MZIMA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE** (Civics, History, Geography, English na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe wamefaulu mtihani wa maarifa (= Q.T.). Masomo yataanza tarehe 18-10-2011. Ada ni Tsh. 160,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 340,000.
10. **KUJIANDAA MWAKA MZIMA KURISITI MTIHANI WA KIDATO CHA NNE** (Civics, History, Geography, English na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe wamefanya ule wa kidato cha nne. Masomo yataanza tarehe 18-10-2011. Ada ni Tsh. 160,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 340,000.
11. **KUJIANDAA HARAKA KURISITI MTIHANI WA KIDATO CHA NNE** (Civics, History, Geography, English na Kiswahili; au Civics, History, Geography na English tu). Wanaotaka kujiunga wawe wamepata credit (A, B au C) walau moja katika somo lolote walipofanya au kurisiti mtihani wa kidato cha nne. Masomo yataanza tarehe 21-2-2012. Ada ni Tsh. 120,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 260,000.
12. **KUJIANDAA MWAKA MZIMA KWA MTIHANI WA KIDATO CHA SITA** (History, Kiswahili na Language; au History, Geography na Kiswahili). Wanaotaka kujiunga wawe wamepata credits (A, B au C) walau tatu katika masomo yoyote walipofanya au kurisiti mtihani wa kidato cha nne. Wawe pia wamepata walau D katika somo la English. Masomo yataanza tarehe 21-2-2012. Ada ni Tsh. 220,000 kwa mwaka. Kwa kukaa bweni wasichana wataongeza Tsh. 360,000.

- Bible Knowledge au Divinity ni somo la lazima kwa Wakristo wa madhehebu yoyote, la hiari kwa wengineo.
- Ada zote zinaweza kulipwa kwa mikupuo minne, isipokuwa ile ya kujiandaa miezi mitatu kwa kidato cha kwanza.
- Ili kukwepa utapeli na ulanguzi, fomu za kujiunga zinapatikana hapa tu kwa Tsh. 10,000 na zinakuwa batili wiki moja baada ya masomo kuanza. Zile za kidato cha kwanza, cha pili, cha tatu na cha nne zinaweza kununuliwa hata siku ya usaili, mradi mtahiniwa alete picha yake ya hivi karibuni.
- Malipo yoyote tofauti na ya fomu yanatolewa risiti katika ofisi ya mhasibu; nje ya hapo si halali, na shule haihusiki nayo, hata kama aliyepewa pesa ni mwalimu.
- Taaluma inadai idadi ya wanafunzi darasani isizidi kiwango fulani, kumbe msongo wa wanaotaka kusoma kwetu ni mkubwa mno: ndiyo sababu ni lazima tuwachuje sana. Kutaka kupokelewa nje ya taratibu zilizopangwa ni kuwadhuru kielimu waliokwishakubaliwa.